JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OR-TAMISEMI)
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIJI
SHULE YA SEKONDARI MKONGO

SIMU: 0686967040 ***S. L. P 40,***
0783330061

IKWIRIRI-

RUFIJI
Email: mkongosecondary@gmail.com

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2022/2023

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa mwanao

……..

amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule ya sekondari Mkongo, tunampongeza kwa mafanikio hayo. Mwanao atatakiwa kuwepo shuleni kwa tarehe itakayokuwa imetangazwa na serikali. Kutofika shuleni kwa wakati uliopangwa kunaweza kumpotezea nafasi yake ya masomo.

Shule ya sekondari Mkongo ipo Mkoa wa Pwani umbali wa kilometa 168 kutoka Dar es salaam. Kwa wanafunzi wa naotoka Mikoa ya kusini (Lindi na Mtwara) washuke kwenye stendi ya wilaya ya Kibiti. Kwa wanafunzi wanaotoka Mikoa mingine wafike **MBAGALA RANGI TATU-DSM,** ndipo watapata magari ya moja kwa moja kuelekea Kibiti, Mohoro,Mohoro na washuke kituo cha mabasi cha kibiti kuna usafiri wa gari mpaka kijiji cha Mkongo. Ambapo umbali wake unakadiriwa kuwa kilometa 30 kutoka Kibiti. Mwanao atapokelewa shuleni endapo atasoma vyema maelekezo na kukubaliana nayo na kutimiza mambo yaliyomo kwenye viambata vifuatavyo **A-G.**

A. Maelekezo ya kujiunga na shule (joining instructions)
B. Ada na michango mbalimbali ya shule
C. Sheria, kanuni na taratibu za shule
D. Maelezo binafsi ya mwanafunzi
E. Fomu ya kupimwa toka kwa mganga (Medical Examination)
F. Ahadi/kiapo cha mwanafunzi
G. Vitabu na vifaa vingine

Ni matumaini yetu kwamba mwanafunzi atasoma na kuzingatia maelekezo yote na mzazi/mlezi utamtimizia mahitaji yote kabla ya kuripoti shuleni ili kuepuka usumbufu usio wa lazima.

MKUU WA SHULE
MKONGO SEKONDARI
S. L. P. 40, IKWIRIRI

MAELEKEZO MAALUM YA KUJIUNGA NA SHULE

1: SARE

Mwanafunzi anatakiwa aje na vifaa/mahitaji yafuatayo

i. Suruali mbili nyeusi
ii. Suruali mbili damu ya mzee
iii. Mashati rangi nyeupe ya mikono mirefu mawili
iv. T.shirt 2 (Fulana zenye nembo ya shule) itapatikana shuleni kwa gharama za mzazi.(wasiliana na uongozi kwa ufafanuzi zaidi)
v. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba vya kufunika visiwe virefu (jozi mbili)
vi. Soksi jozi 2 au zaidi nyeusi/Dark blue
vii. Viatu vya michezo
viii. Kandambili kwa ajili ya kuogea tu
ix. Track suit (jezi za michezo) rangi ya blue zisizo na maandishi.

2: MAHITAJI YA BWENI

i. Godoro la futi $2^1/_2$ kwa 6
ii. Shuka 3 rangi ya blue bahari
iii. Neti ya mbu 1
iv. Mto na foronya mbili rangi ya blue bahari
v. Taulo
vi. Nguo za ndani za kutosha
vii. machine ya kunyolea ndevu(sio ya umeme)
viii. Ndoo ndogo 2 za lita kumi
ix. Sanduku imara la bati moja lenye makufuli mawili
x. Vyombo vya chakula (sahani,bakuli, kikombe, kijiko, chupa ya chai anaweza kuja na hot pot 1 ndogo kwa ajili ya dharura za kiafya visivyo vya plastiki)

3: MAHITAJI YA TAALUMA.

i. Picha 4 pps akiwa amevaa shati jeupe na rangi ya blue nyuma ya picha
ii. Rimu 1 kwa mwaka A4 aina ya ROTATRIM, NOPATOP AU MONDI PEKEE.
iii. Result slip ya kidato cha nne (CSEE) halisi na nakala
iv. Cheti cha kuzaliwa halisi na nakala
v. Cheti cha kumaliza kidato cha nne (leaving certificate) halisi na nakala.

4: MAHITAJI DARASANI.

i. Madaftari (kaunta books) 10.
ii. Kalamu na penseli za kutosha.
iii. Mkebe wa hisabati (Mathematical set)
iv. Mikasi (Dissection kit) kwa ajili ya kupasulia (masomo ya sayansi pekee)
v. Scientific calculator
vi. Koti la maabara (Laboratory coat) kwa wanaochukua masomo ya sayansi

B: ADA NA MICHANGO MBALIMBALI

Ada na michango mbalimbali ni kama ifuatavyo;-

JEDWALI LA AINISHO LA ADA NA MICHANGO KWA KIDATO CHA TANO

Na.	MICHANGO	MUHULA 1	MUHULA 2	JUMLA
1	ADA	35,000/=	35,000/=	70,000/=
2	TAHADHARI	5000/=		5,000/=
3	ULINZI NA UPISHI	30,000/=		30,000/=
4	HUDUMA YA KWANZA NA BIMA YA AFYA	10,000/=		10,000/=
5	UKARABATI WA SAMANI	15,000/=		15,000/=
6	MITIHANI YA KUJIPIMA	20,000/=		20,000/=
7	NEMBO YA SHULE	2,000/=		2,000/=
8	TAALUMA	20,000/=		20,000/=
9	KITAMBULISHO NA PICHA	6,000/=		6,000/=
JUMLA				178,000/=

- ADA ilipwe kwenye akaunti namba **21301100051 NMB BANK** jina la akaunti ni **MKONGO SECONDARY SCHOOL RECURRENT**.
- Michango mingine yote ilipwe kwenye akaunti namba **21301100007 NMB BANK** jina la akaunti ni **MKONGO SECONDARY SCHOOL FUND.**

NB: Kuwa makini katika kuweka fedha katika akaunti za shule, fedha za ada ziwekwe kwenye akaunti ya ada tu, na michango mingine yote iwekwe kwenye akaunti ya michango na si vinginevyo. Hatutahusika na uzembe wowote wa kuchanganya malipo katika akaunti za shule. Jina la mwekaji liwe la mwanafunzi na si mzazi/mlezi. Mwanafunzi aje na **PAY SLIP** ya benki wakati wa kuripoti.



SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Sheria na kanuni hizi zinazingatia misingi ya **HESHIMA, ADABU, UAMINIFU, UTII** na **TABIA NJEMA** kwa ujumla.

SHERIA KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Sheria na kanuni hizi zinazingatia misingi ya heshima, adabu uaminifu, utii na tabia njema kwa ujumla

Mwanafunzi anatazamiwa kuwa mfano mzuri kwa heshima na tabia na kauli na vitendo, hivyo:

i. Mwanafunzi atasimama anapomsalimia mwalimu, mtumishi wa shule au mtu yeyote anayemzidi umri
ii. Hairuhusiwi kwa mwafunzi kutumia lugha chafu nay a kihuni popote na wakati wowote hata kwa wanafunzi wenzake.
iii. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi
    A. Kuvuta sigara na kutumia madawa ya kulevya
    B. Kufuga nywele na kucha
    C. Kufuga ndevu
    D. Kunyoa kipara
    E. Kumpiga mwezake
    F. Kutukana
    G. Kutia dawa nywele (curly) na kujichubua ya mwili kwa madawa
    H. Kuchora tatuu kwa namna yeyote ile
    I. Kuvaa vitu kama mapambo kama vile; Heleni,, Bangili au vitu vya kiimani kama vile Rozali, KOFIA, KANZU, VILEMBA, SURUALI FUPI kwa kuwa shule hii ni serikali
    J. Kuvaa viatu vya sori nene na ndefu
    K. Kuvaa kaptura, kandambili kwenye bwalo la chakula na ofisi zote.
    L. Kuvaa suruali chini ya kiuno
iv. Mwanafunzi asimama kwenye mstari wakati wa kupata huduma
v. Mwanafunzi atanyoosha mkono juu na kusimama anapouliza na kujibu swali
vi. Anatakiwa kuwa mtulivu asipige kelele au vitendo vyovyote vitakavyosababisha usumbufu kwa wengine anapokuwa darasani, maktaba, hostel, wakati wa kujisomea na katika mikusanyiko yote mfano pared n.k
vii. Mwanafunzi lazima awahi na ahudhurie mahali anapotakiwa katika shughuli za shule. Mwanafunzi;
    A. Aripoti shuleni tarehe ya kungua shule na kujiandikisha rasmi siku na saa ya kuripoti kwa mwalimu anayehusika.
    B. Ahudhurie vipindi vyote darasani kama ilivyopangwa
    C. Ahudhurie kwenye kazi atakazopangiwa
    D. Ahudhurie kwenye paredi ya uhakiki wa uwepo wake shule (roll call). Ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa, mikutano ya hostel na bweni na mikutano ya darasa
viii. Ni lazima mwanafunzi awe katika sare ya shule na awe na kitambulisho kwa nyakati zote awapo shuleni na nje ya shule. MAVAZI YA NYUMBANI HAYARUHUSIWI KABISA
ix. Haruiruhusiwi mwanafunzi kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa mfano kwenda kanisani, msikitini, Benki, Hospitali, likizo au kwa shughuli yeyote inayomlazimu kwenda nje ya shule.

x. Mwanafunzi nilazima ahudhurie prep inayoanza saa 1:30 jioni hadi saa 4:30 usiku na prep ya saa 11:00 asubuhi kwa wale waishio hostel

xi. Mwanafunzi anahaki na wajibu wa kuchagua au kuchaguliwa kuwa kiongozi wa wanafunzi wenzake.

xii. Mwanafunzi haruhusiwi kujipikia hostel au bwenini wala kutumia electrical heater au jiko la aina yoyote.

xiii. Hairuhusiwi kufanya mikutano yoyote shuleni pasipo kibali kutoka kwa mkuu wa shule na ikiwa kibali kitatolewa kikundi au chama kitatatkiwa kuandika muhtasari wa kikao na nakala kuwasilisha kwa mkuu wa shule.

xiv. Usafi; mwanafunzi anawajibika kuwa msafi kwa mavazi na mwili wake na kushiriki kuyaweka mazingira ya shule safi.

xv. Hairuhusiwi mwanafunzi kumiliki ***SIMU AU SEHEMU YA SIMU KAMA VILE LAINI,CHARGER,EAR PHONE,IPAD n.k***

xvi. hairusiwi kujihusisha na mikutano ya siasa katika kipindi chote awapo mwanafunzi

xvii. MAENEO YASIYORUHUSIWA

A. Ofisi za shule
B. Bohari za shule
C. Kwenye disco, ngoma, mziki au kwenye sherehe yeyote nje ya shule
D. Baa, kilabu au mahali popote panapouzwa pombeau vile vingine.
E. Maabara
F. Nyumba za wageni
G. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kuuza, kutumia au kubeba pombe, bangi au vile vingine
H. Nyumba za watumishi /walimu

MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE

1. Wizi
2. Kugoma na kuhamasisha mgomo
3. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
4. Uvutaji wa sigara.
5. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
6. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wantakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
7. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
8. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, Kuoa au kuolewa
9. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yeyote yale yanayovunja sheria za nchi.
10. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.
11. Kudharau bendera ya Taifa
12. Kufuga ndevu.
13. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
14. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
15. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
16. Kutohudhuria asomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
17. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

VITABU NA VIFAA

1. GEOGRAPHY
   I. Physical geography (Monk House)
   J. Practical geography for Africa by john Richard
   K. Fundamental geography by josephat Mwita
   L. Human economic Geography by Msabila

2. KISWAHILI

Kila mwanafunzi aliyepangwa kuja kusoma somo la Kiswahili anatakiwa kuja na angalau vitabu viwili kati ya vifuatavyo

- Samakisa na Samikisa (Masamba na wenzake)
- Kiswahili kidato cha tano na sita (oxford)
- Nadharia ya fasihi ya Kiswahili 2 (nyambari nyangwine)
- Tafsiri na ukarimani (mwansoko)
- Kamusi ya Kiswahili sanifu (TUKI) lazima aje nayo

Vilevile aje na vitabu viwili viwili katika riwya, mashairi na Tamthiriya. Chagua hapo chini kwenye orodha

USHAIRI

- KIMBUNGA (HAJI GORA)
- MAPENZI BORA (SHABANI ROBERT)
- CHUNGU TAMU (THEOBALD MVUNGI)
- FUNGATE YA UHURU (MOHAMEDI S. KHATIBU)

RIWAYA

- ✓ USIKU UTAKAPOKWISHA (MBUNDA MSOKILE)
- ✓ KUFIKIRIKA (SHABAN ROBERT)
- ✓ MFADHIRI (HUSSEIN TUWA)
- ✓ VUTA N KUVUTE (SHAFI ADAM SHAFI)

TAMTHILIYA

- ❖ KWENYE UKINGO WA THIM (EBRAHMI HUSSEIN)
- ❖ MORANI (EMMANUEL MBOGO)
- ❖ NGUZO MAMA (PENINA MHANDO)
- ❖ KIVULI KINAISHI (SAID MOHAMED)

3. HISTORY

Kwa anayesoma histori tu, aje na vitabu japo viwili kati ya vifuatavyo

- Essential in advanced level History paper 1 by Salehe Yasin
- Advanced history paper 1 by zist Kamili
- The evolving world by Denis Ngalula
- Advanced level History paper 2 By Pascrates fidelis Rutta

4. ENGLISH LANGUAGE

- ❖ Advanced English Dictionary 7th edition lazima aje nayo

- Advanced level English language (structure and stylistics) by N. asheli
- Contemporary English for advanced level by Francis Myawi

Mwanafunzi anatakiwa kuja pia na vitabu angalau viwili vya PLAY viwili NOVELS

NOVELS

- Divine providence (severin N Ndunguru)
- Encounters from Africa (macmilian Education limited)
- His excellency the head of state (Danny Safo)
- The beautiful ones are not yet born (Ayi Kwei Arman)
- A man of the people (Chinua Achebe)

PLAY

- Betrayal in the city (Francis Imbugha)
- I will marry when I want (Ngugi wa Thiong'o)
- The bride (Austin Bukenya)
- An enemy of the people (Henrick Ibsen)
- Black Mamba (John Luganda)

5. BIOLOGY

- Biological science (D.j Taylor)
- Understanding biology for advanced level by Grenn & Sasan Toole
- Biology a function approach 4th Edition By M.B.V Roberts
- Modern ABC Biology class XII part I & II by Dr B.B ARORA
- S. CHAND'S biology for class XI & XII By Dr. P.S VERMA

6. CHEMISTRY

- Modern chemistry ABC Of class XI Part I & II By Dr. S.P Jauhar
- Modern chemistry ABC Of class XII Part I & II By Dr. S.P Jauhar
- Physical chemistry by Chan

7. GENERAL STUDIES

Kila mwanafunzi lazima aje na kitabu cha somo la General studies kati ya

General studies by ZISTI KAMILI

Simplified General studies by Nyambari Nyangwine

8. **BASIC APLIED MATHEMATICS** kwa CBG pekee

BASIC APPLIED MATHEMATICS by MAT

VIFAA

Vifaa vya usafi ni lazima kwa kila mwanafunzi, vifuatavyo ni lazima aje navyo na kukabidhi shuleni anaporipoti.

VIFAA

1. Fagio la chelewa lenye mpini 1
2. Fagio la ndani i.e hard broom/ soft broom 1
3. Fyekeo(kwanja) 1
4. Jembe lenye mpini 1
5. Reki 1

OFISI YA RAIS- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OR-TAMISEMI)

HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIJI

SHULE YA SEKONDARI MKONGO

C. KIAPO CHA MWANAFUNZI

Mimi ……. Ambaye nimechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Mkongo kidato cha …….. mwaka …… ninaikubali na kuipokea nafasi hii niliyopewa kwa malengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo ya Taifa na shule ya mkongo sekondari.

Ninatambua kuwa kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti nay a upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya Taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwa ajili yangu pia.

Ninaamini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu, familia yangu na kwangu pia. Hivyo ninaahidi kuwa nikiwa hapa shuleni

1. **Nitasoma kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo yangu**
2. **Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyozisoma na kuzielewa na zingine zitakazokuwa zikitolewa mara kwa mara.**
3. **Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapa shuleni**
4. **Ikiwa nitakiuka sheria, kanuni na taratibu za shule kama nilivyozisoma na kuzielewa, nitakubali kurudi nyumbani kumwita mzazi/mlezi wangu …….. (jina la mzazi)kwa ajili ya hatua stahiki za kinidhamu**

Sahihi ya mwanafunzi …… tarehe …….

SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

Mmi …… ninakubali mtoto wangu ……. Kupata na kupokea nafasi katika shule ya sekondari Mkongo mwaka …… ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyokatika maagizo ya kujiunga na shule . ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa Taifa

ANUANI YANGU ……. SIMU NA ……

SAHIHI ……..

TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi …… adm No ……
2. Kidato …….. Mchepuo …….. mwaka ……..
3. Tarehe na mwaka wa kuzaliwa …….
4. Kabila la mwanafunzi ……..
5. Uraia wa mwanafunzi ……
6. Tarehe ya kujiunda na shule ya sekondari mkongo
7. Shule ya sekondari atokayo mwanafunzi ……
8. Kama ni mlemavu, taja aina ya ulemavu …….
9. Je unarudia kidato? ……. Kwa nini ……
10. Dini ya mwanafunzi …… dhehebu ……
11. Bweni atakalopangiwa …….
12. Anuani nya kudumu ya mwanafunzi
    Wilaya…… mkoa……
    Tarafa ……. Kata ……
    Kijiji …….
    Simu ya nyumbani ……

BABA

13. JINA LA BABA ……
14. Je yu hai? ……..
15. Kabila la baba ……
16. Anuani yake ya sasa …….
17. Kazi yake …….
18. Mwajiri wake ……
19. Dini ya baba …….. dhehebu …….
20. Je baba na mama wanaishi pamoja ……
21. Simu ya baba ……. Ya kazini ……

MAMA

22. Jina la mama ……
23. Je yu hai? ……
24. Kabila la mama……
25. Anuani yake ya sasa …….
26. Kazi yake …….
27. Mwajiri wake ……
28. Dini ya mama…….. dhehebu …….
29. Simu ya baba ……. Ya kazini ……

MLEZI

30. Jina la mlezi ……
31. Kabila la mlezi……
32. Anuani yake ya sasa …….

33. Kazi yake …….
34. Mwajiri wake ……
35. Dini ya mlezi…….. dhehebu …….
36. Simu ya mlezi ……. Ya kazini ……

NDUGU WENGINE

JINA	ANUANI	SIMU

HABARI NYINGINE

……..

SAINI

Sahihi ya mwanafunzi

……..

Jina la mwalimu wa darasa

…….

Sahihi ya mwalimu wa darasa

……..

PRESIDENT OFFICE

REGIONAL ADMINISTRAN AND LOCAL GOVERNMENT (PO-RALG)

MKONGO SECONDARY SCHOOL

SIM: 0686967040

0682362910

P.O BOX 40,

IKWIRIRI-

RUFIJI

DATE ……

STUDENT MEDICAL EXAMINATION FORM

To the medical officer ……
……
……
……
……

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF …….
FORM ……. YEAR ……
Please examine the above named as to his fitness for admission to school as a student.

Name and signature of requesting officer
Name …….. Signature ……
Date ……

(*To be completed by a medical officer*)
I have examined the above named and she/he has found with ……
……
…… I consider that he/she-- is physically fit/unfit to pursue as stated above

(*Name and signature of certifying officer*)

Name …….. Signature ……

Station …….. STAMP……..
Date ……..